# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**FRIENDS SCHOOL KAMUSINGA HIGH**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 1**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

# FRIENDS SCHOOL KAMUSINGA KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/1**

**Karatasi ya I**

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SWALI LA KWANZA**
**Muundo wa ripoti rasmi uzingatiwe.**

- Kichwa – kiwe kwa herufi kubwa
- Utangulizi – Historia fupi ya suala linalotafitiwa itolewe ikiwa ni pamoja na kutaja wanajopo watano na muda wa kutafiti.
- Yaliyoshughulikiwa – Taratibu za kufanyia utafiti ziorodheshwe. Hizi ndizo zitafuatwa baadaye katika mwili wa insha.
- Mwili/matokeo ya uchunguzi. Haya ni masuala yaliyoshughulikiwa na jopo pamoja na utaratibu uliofuatwa katika kutafiti yale yaliyoagizwa.
- Matatizo; iwapo jopo lilikumbana na matatizo yoyote, matatizo hayo huorodheshwa chini ya kijianwani cha matatizo.
- Hitimisho: sifa za ripoti zirejelewe.
- Mapendekezo: Jopo litoe msimano wake baada ya kukamilisha utafiti.
- Jina, sahihi na cheo cha mtayarishi pamoja na tarehe ziandikwe.

  Tanbihi: Mtahiniwa asipofuata sura ya ripoti rasmi, aondelewe alama 4.

<u>Vidokezo</u>

A. <u>Sababu za undanganyifu</u>

- Kukosa kujiandaa ipasavyo kabla ya mtihani.
- Uzembe wa wanafunzi katika kujiandaa masomoni.
- Baadhi ya wazazi huwa wakali sana kwa watoto wao wasiofanya vyema masomoni.

- Wazazi wengine kutaka watoto wao wajiunge na vyuo vikuu kwa njia yoyote ile.
- Ufisadi kuwa wa hali ya juu kiasi kwamba walioaminiwa kuweka siri katika mitihani kuhongwa na kutoa nakala za mitihani hiyo.
- Ni njia ya kuchumia mali kwa watu wengine kwani soko i tayari ya mitihani.
- Mashindano miongoni mwa shule
- Wakuu wengine kutaka sifa baada ya matokeo ya mitihani.
- Limekuwa kama jambo la kawaida katika baadhi ya maneo fulani.
- Teknolojia mpya – matumizi ya simu na mtandao.

B. <u>Madhara ya undanganyifu</u>

- Matokeo ya mitihani kwa jumla kuathiriwa vikali kwani viwango vingine vya alama huwekwa juu sana.
- Watu wengine huishia jela kwa kujihusisha na undanganyifu huu.
- Watahiniwa waliohusika kukosa matokeo ya mitihani.
- Wanafunzi wasio na hatia huathirika kwa matokeo yao ya mitihani.
- Kukosa imani kwa taasisi ya kushughulikia mitihani nchini (utunzi na usahihishaji)
- Wasiostahili kujiunga na vyuo vikuu na kuwanyima haki wanaostahili.
- Mitihani bandia kuingia sokoni kwa madai kuwa ni ya kweli.
- Matokeo mabaye baada ya kudanganya hufanya wanafunzi wengine kujitoa uhai.
  n.k

c. <u>Jinsi ya kukabiliana na undanganyifu (suluhisho)</u>

- Wanafunzi walenge kupata alama kulingana na uwezo wao.
- Wazazi wawe na matarajio ya matokeo ya mitihani kulingana na uwezo wa watoto wato.

- Shule zishindane kulingana na kiwango chao masomoni.

- Walimu watayarishe watahinwa vilivyo.

- Mfumo wa elimu ufanyiwe marekebisho ili usiegemee kupita mitihani pekee, bali uangazie vipawa vya wanafunzi katika nyanja zingine k.v. michezo, sanaa, nyimbo n.k.

- Wasimamizi wa shule, mitihani na walimu kwa jumla wawe macho wakati wa mitihani.

- Hatua kali zichukuliwe kwa wale watakaojihusisha na undanganyifu n.k

  <u>Tanbihi</u>
  Zingatia hoja zingine za watahiniwa

1. Katika kujibu swali hili, mtahiniwa anaweza:

a) Kuunga mkono kauli hii

b) Kupinga kauli hii

c) Kuunga na kupinga kisha atoe msimamo wake.

<u>Vidokezo.</u>
<u>Kuunga mkono</u>
<u>Changamoto za usalama.</u>

- Magaidi wanaweza kutokea popote na kuvamia watu bila tahadhari.

- Raia kuwa na hofu wanapotekeleza majukumu yao ya kila siku.

- Watu kupoteza maisha yao uvamizi unapotokea.

- Vijana kutekwa nyara na kuingizwa katika makundi ya kigaidi.

- Vijana kuingizwa katika makundi ya kigaidi na kuzorotesha usalama zaidi.

- Watalii wa kigeni kuhofia kutalii nchini.

<u>Changamoto za maendeleo</u>

- Serikali kutumia kiasi kikubwa cha rasilmali kuajiri askari wa kulinda usalama.

- Maeneo yanayoaminika kuwahifadhi magaidi hawa kukosa wahudumu.

- Watu kupoteza mali wakati wa mashambulizi.

- Wawekezaji kuwa na uoga kufanya biashara nchini.

- Serikali kulazimika kuchukua hatua zenye gharama

- Kubwa kuzuia ugaidi k.v.

    - Ujenzi wa ua kwenye mipaka ya nchi jirani

    - Mafunzo ya kikosi cha walinda usalama, pamoja na mishahara yao.

    - Ununuzi wa magari ya kulinda usalama.

2. Hii ni insha ya methali
   Mtahiniwa anaweza kufahamu methali kimaana na kimatumzi (si lazima) kilicho muhimu ni kisa kinachoonyesha ukweli wa methali hii.

- <u>Mwenye kovu</u> – Mtu aliyewahi kukumbwa na jambo fulai baya/lenye kuumiza/lenye kusababisha uchungu fulani.

- <u>Sidhani kapoa</u> – usichukulie kuwa amesahau jambo lile na kutulia.

- <u>Maana</u>
  Mtu aliyewahi kubumbwa na jambo lenye kutia uchungu atabaki akilikumbuka hasa kwa hasira.
  Atakuwa akitafuta nafasi ya kupiliza kisasi hasa ikiwa jambo lile lilisababishwa na mtu anayemjua.

  <u>Tanbihi</u>
  Kisa kionyeshe hali ya kulipiza kisasi kwa uovu aliotendewa mtu.
  Mtahini akikosa kutunga kisa kitakachooana na methali, hajajibu swali.

4. Ni lazima mtahiniwa akamilishe insha yake kwa maneno haya. Sentensi yenye mdokezo iwekewe maneno ya kwanzia ili itiririke vyema.
   Kisa kidhihirishe kuwa mwanafunzi alipuuza ushauri/wasia wa mwalimu na hatimaye akajutia mapuuza hayo.